**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**

**26.09.2025**

**TANGAZO LA AJIRA ZA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anapenda kuwatangazia Watanzania Wote kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imekusudia kuajiri Watumishi wa Mkataba wa kazi ya Muda ya **Dereva Daraja la II** na **Fundi Sanifu Mitambo (Mechanical Technician II)** ambao watafanya kazi katika **Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.**

**DEREVA DARAJA LA II NAFASI (08)**

**1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA**

i. Awe amehitimu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) na kufaulu.
ii. Awe na Leseni Daraja C au E ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na NIT, Veta au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iv. Mwombaji awe na cheti cha majaribio ya ufundi Daraja II (Trade Test Grade II).

**1.2. KAZI ZA KUFANYA**

I. Kuendesha magari ya Abiria na Malori.
II. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri na usafi wakati wote na kufanya Uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
III. Kufanya matengenezo madogomadogo katika gari.
IV. Kutunza na kuandika daftari la Safari "Log – book" kwa Safari zote.
V. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri wako.

**1.3. MALIPO YA AJIRA KWA NAFASI YA DEREVA DARAJA LA II**

Mshahara kwa mwezi ni **Tsh. 350,000/=**

**FUNDI SANIFU MITAMBO (MECHANICAL TECHNICIAN) DARAJA LA II NAFASI MOJA (01)**

**1.4. SIFA ZA FUNDI SANIFU MITAMBO (MECHANICAL TECHNICIAN) II**

i. Awe na Diploma ya Mechanical au Automobile.
ii. Awe na FTC ya Mechanical au Automobile.
iii. Awe na kozi ya Tred Test one, two au three kwa kozi ya Mechanical au Automobile.
iv. Awe na uzoefu wa UFUNDI MAGARI usiopungua miaka 3.
v. Awe Raia ya Tanzania.

**1.5 KAZI ZA KUFANYA.**

i. Kufanya Matengenezo madogo na makubwa ya magari, mitambo na genereta ya Halmashauri.
ii. Kufanya ukaguzi wa magari, mitambo na generetor za Halmashauri na kutoa taarifa kwa Mkuu wake wa kazi.
iii. Kuandaa taarifa mbalimbali zinazohusu matengenezo ya magari, mitambo na generetor
iv. Kufanya kazi zote atakazopangiwa Mkuu/Msimamizi wake wa kazi.

**1.6. MALIPO YA AJIRA KWA NAFASI YA FUNDI SANIFU MITAMBO (MECHANICAL TECHNICIAN) DARAJA LA II**

Mshahara kwa mwezi ni **Tsh. 350,000/=**

**1.7. MASHARTI YA JUMLA**

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.
ii. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
iii. Maombi yote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)
iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
v. Testmonials","Provisional Results","Statement of results", hati ya matokeo za kidato cha nne na sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA).
vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa UMMA hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wanakibali cha katibu Mkuu kiongozi.
viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
ix. Awe na Kitambulisho au namba ya Utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
x. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **09.10.2025** saa **9.30 Alasiri.**
xi. Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yawasilishwe Masjala ya wazi ofisi Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Barua zote ziandikwe kwa anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA,**
**S.L.P 599,**
**MBEYA.**